SOMO LA SITA



YESU ALIWAPA WAJIBU GANI WANAFUNZI WAKE?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

LAZIMA WAWAITE WOTE KUTUBU

" Nenda ulimwenguni kote! "

Yesu alionekana akiwa hai kwa wanafunzi Wake katika matukio mengi na akawaeleza kwa kurudia kuwa ilikuwa muhimu Kwake kufa na kufufuka kutoka kwa wafu.[1] Aliwaambia pia kutangaza msamaha, kupitia kifo Chake, kwa ulimwengu wote[2] wakianzia Yerusalemu. Wokovu huu wa bure hupatikana kwa sharti la kugeuka kutoka dhambini na kuamini katika Kristo.

Agano Jipya hutuambia kuwa Yesu hatimaye alipokelewa tena Mbinguni katika mawing[3] na akaketishwa katika mkuno wa kuume wa Mungu.[4]

NI LAZIMA WAWAITE WOTE KUTUBU

Yesu aliwaamuru wanafunzi Wake kuwaambia watu yote popote ili wageuke kutoka njia zao za dhambi.[5] Huku ndiko kutubu. Mtu wa kwanza kutangaza toba baada ya Yesu kufufuka alikwa Petro, mmoja wa wanafunzi maarufu.

Alihubiri msamaha (kwa imani katika Kristo) kwao waliokuwa Yerusalemu waliomuua Yesu – lakini ni lazima kwanza watubu dhambi zao.
Angalia Matend 2:38

Kama mwovu anaweza kuokolewa, nami naweza.

.....

.....

.....

.....

ASILI YA KWELI YA TOBA

Toba ya kweli huanzia utambuzi wa ndani wa makosa ya mtu binafsi. Angalia jinsi walivyojutia dhambi zao baada ya Petro kuwahubiri.

Tazama Matendo 2:37

.....

.....

.....

.....

Walichomwa mioyo

[1] Luka 24:25-27, 44-46
[2] Roho wa Mungu atawapa ujasiri kwa ajili ya hatua hii kuu. Angalia Matendo 2:1-4
[3] Matendo 1:9-11
[4] Matendo 5:31
[5] Luka 24:46-47

Kuishi kwa mabadiliko

Lakini toba ya kweli ni zaid ya kuhurumiwa dhambi zetu; ni utambuzi[6] na kuamua kuacha dhambi. Toba nyakati zote huambatana na mabadiliko ya maisha.[7] Tazama Matendo 26:20

.....

.....

.....

.....

.....

Punde tu dhambi inapotubiwa na kuachwa, kuna hali moja tu inayobaki kwa ajili ya wokovu. Ni imani katika Kristo (inayofuata).

Walitii amri Yake

NI LAZIMA KUWAITA WOTE KUAMINI

Yesu aliwaamurisha wanafunzi Wake kumtangaza katika ulimwengu ambao hujawahi Kumwona. Na pamoja na kuwa hawajawahi kumwona Yesu, lazima kuamini ushuhuda wa waliomwona.[8]

Siyo kwamba lazima waamini juu ya Yesu, ila pia waamini kwa kumgeukia katika wokovu aliouleta kwa kifo Chake ili kuwapatanisha na Mungu. Imani katika Kristo ni hatua ya pili kwa ajili ya wokovu.

LAZIMA KUWAALIKA WOTE KUAMINI

Mwanafunzi Yohana aliandika “Injili ya Yohana” ili wasomi watakaoisoma Injili waweze kuamini. Tazama Yohana 20:31

.....

.....

Kutangaza habari Njema

.....

.....

Paulo alikuwa kiongozi wa kanisa ambaye alifungwa kwa makosa. Alihubiri Injili kwa askari wa jela. Alimwambia amwamini Kristo kwa ajili ya wokovu. Tazama Matendo 16:31

.....

.....

.....

ASILI YA KWELI YA IMANI IOKOAYO

Mtu anayepotea hawezi kujiokoa

Mtu mwenye Imani ya kuokoa huamini Kifo cha Yesu pekee kumweka sawasawa na Mungu.[9] Mtu mnyenyekevu ni lazima kwanza aondoe tumaini la kujiokoa binafsi, na kuamini mwingine kumwokoa. Wale wanaoamini wema wao kuwaweka sawasawa na Mungu hawaamini msalaba kuwawaokoa.

---

[6] Luka 15:21

[7] Zingatia Luka 3:7-8

[8] Yohana 20:29

[9] Siyo tu imani yoyote itaokoa wenye dhambi. Hata mapepo huamini (Yakobo 2:19).

Msamaha ni kwa imani tu, siyo kwa matendo mema,[10] vinginevyo mtu yeyote angejisifu. Tazama Waefeso 2:8-9

Hakuna nafasi ya kujivuna

.....

.....

.....

.....

Imani ya kweli inapelekea matendo. Kama kweli tutaamini jingo linawaka moto tutaondokamo haraka. Na kama kwa hakika tukiamini kuwa Mungu anachukia dhambi tutajitahidi tuwezavyo kuiacha. Imani bila matendo imekufa. Imani ya kweli itajulikana jinsi tuishivyo. Soma Yakobo 2:17-18. Andika Yakobo 2:18.

Lazima nitende nikijuacho.

.....

.....

.....

.....

Imani siyo wozo ndani ya akili, au usemi ulioandikwa wa mafundisho. Ni uhakika imara wa ndani[11] ambao hauaibishi kuwa na Kristo mbele ya wengine.[12]

LAZIMA WAWABATIZE WANAFUNZI WAPYA

Ubatizo wa siku mpya

Kabla Yesu hajawaacha wanafunzi wake kurudi Mbinguni, Aliwaambia wawabatize wale watakaomwamini kama matokeo ya mahubiri yao ya Injili. Hili litakuwa ndiyo kawaida ya kanisa. Lakini wasiopenda kutubu na kuamini, ubarizo ulikuwa siyo sharti la wokovu.

UBATIZO NI JARIBIO LA UTII

Petro alipomhubiri Kristo, aliwaambia wale waliaoamini kuwa watubu na kubatizwa (angalia Matendo 2:38 ukurasa wa 21). Alifanya hivyo kwa sababu Yesu ameamuru waamini wabatizwe. Waamini wa kweli watahitaji kumtii Mwokozi wao na kubatizwa. Tazama Mathayo 28:19

.....

.....

.....

UBATIZO NI ISHARA YA KUOSHWA KABISA DHAMBI [13]

Hakuna sikukuu inayoweza kuondoa dhambi

Wale waliobatizwa na Petro na Paulo walikuwa tayari ni Wakristo. Hawakuwa Wakristo kwa sababu ya kubatizwa. Ubatizo ni ishara ya kile alichokifanya Kristo tayari kwa ajili yao – dhambi zao tayari zimeoshwa. Soma 1 Wakorintho 6:9-11.

[10] Wokovu ni zawadi, haiwezi kupatikana kwa matendo yetu (Warumi 6:23).
[11] Waebrania 11:1
[12] Warumi 10:9-10
[13] Angalia somo “Kuanza kama Mkristo” kwa udhibitisho zaidi wa Ubarizo.

Andika 1 Wakorintho 6:11.

.....

.....

.....

.....

Ubatizo hauwezi kusafisha dhambi, damu ya Kristo pekee inaweza. Angalia itifaki.[14]

Kuchukua nafasi ya uamuzi wetu!

LAZIMA WAMHUBIRI KAMA MUHUKUMU WA DUNIA

Moja ya maelekezo aliyoyatoa Yesu mara nyingi yameachwa. Wanafunzi waliambiwa kuambia ulimwengu kuwa Yesu ndiye muhukumu wa siku zijazo. Ndiyo, mtu pekee aliyekuja kuuokoa ulimwengu atarudi kuuhukumu! Hii ni tahadhari iliyotolewa, na inpaswa kutushawishi kupatana na Mungu sasa, wakati tuna nafasi.

YESU MUHUKUMU WA ULIMWENGU

Kati ya mafundisho ya Yesu yalikuwa juu ya wajibu wake wa kuuhukumu baadaye. Hivyo haishangazi kuwa Yesu alitoa amri hii. Angalia Matendo 10:42

.....

.....

.....

.....

Atakuwa wa haki

YESU MUHUKUMU WA HAKI

Yesu kwa haki atawalaumu wale ambao hawakutubu, kwa kuwa Yeye ni wa haki kwa kuhukumu bila upendeleo. Angalia Matendo 17:31

.....

.....

.....

.....

.....

HITIMISHO

Kumbuka: imani hupelekea matendo!

Agano Jipya ni orodha ya ya maajabu ambayo Mungu ameyafanya ili kuwapatanisha wenye dhambi kwake Mwenyewe. Hatahivyo, waandishi wametuonya juu ya kudharau yale aliyoyatenda Mungu.[15] Sasa ni wakati wa kutenda – "sasa ni wakati uliokubalika; tazama, siku ya wokovu ni leo."[16]

Ni makosa na hatari kwa kuweka mbali wajibu wetu kusubiri wakati mwingine. Tutatoa udhuru wa namna gani kwa Mungu Mkuu ili aendelee kusubiri? Kama hatujageuka kuiacha dhambi, na kumwamini Kristo kama Mwokozi, tunatakiwa kufanya hivyo sasa. Hatupaswi kukwepa. Yesu alisema kama hatuko upande wake sisi tuko kinyume Naye.[17]

---

[14] Ufunuo 1:5. Pia Matendo 22:16, ambayo huonyesha *ishara* yenye maana ya ubatizo.

[15] Waebrania 2:3

[16] 2Wakorintho 6:2

[17] Mathayo 12:30